AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi: +251 115 517 844
Tuvuti : www.au.int


**BARAZA KUU**
**Kikao cha Arobaini na nne cha Kawaida**
**Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**


**EX.CL/1486(XLIV)A**
Matini chanzi: Kiingereza


# TAARIFA YA MAENDELEO JUU YA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA WAKALA WA DAWA AFRIKA

# TAARIFA YA MAENDELEO JUU YA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA WAKALA WA DAWA AFRIKA

**Tarehe 1 Januari 2023 - 31 Desemba 2023**

**Ripoti hii ina sehemu nne:**

i. Sehemu ya 1: Ripoti ya Maendeleo ya Kuanzishwa na Uendeshaji wa Wakala wa Madawa wa Afrika

ii. Sehemu ya 2: Rasimu ya Uamuzi kuhusu Ripoti ya Maendeleo ya Wakala wa Dawa wa Afrika (AMA) ya 2023

## Sehemu ya 1. Ripoti ya Maendeleo ya Kuanzishwa na Uendeshaji wa Wakala wa Madawa wa Afrika

## I. Utangulizi

1. Mkataba wa Kuanzishwa kwa Wakala wa Dawa wa Afrika (AMA) ulipitishwa tarehe 11 Februari 2019 wakati wa Kikao cha 32 cha Kawaida cha Halmashauri Kuu ya Afrika (AU), mjini Addis Ababa, Ethiopia (Assembly/AU/Des.735(XXXII)) Mkataba wa AMA ulianza kutumika tarehe 5 Novemba 2021 kufuatia kuwekwa kwa hati ya 15 ya uidhinishaji. Kuanza kutumika kwa haraka (miaka 2 na miezi 9) imesalia kuwa rekodi katika kumbukumbu za Tume ya Umoja wa Afrika. Zaidi ya hayo, hitaji la dharura na umuhimu wa kuwa na wakala wa udhibiti wa dawa wa bara haujaonyeshwa tu katika idadi ya uidhinishaji wa Mkataba wa AMA, lakini pia katika maendeleo yaliyoonekana kwenye utendaji kazi wa AMA. AMA iliyoanzishwa kama wakala maalumu wa Umoja wa Afrika itaimarisha uwezo wa Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), kudhibiti na kuboresha upatikanaji wa dawa bora, salama na zinazofaa, bidhaa za matibabu na teknolojia barani Afrika. Zaidi ya hayo, itaratibu mipango na mifumo ya udhibiti inayoendelea katika bara la Afrika.

## II. Usuli

**2.** Afya na ustawi wa Waafrika umeangaziwa kama msingi wa ujenzi ili kufikia mabadiliko ya kijamii na kiuchumi na kimuundo kama inavyotarajiwa katika Ajenda ya Afrika ya 2063. Aidha, imesisitizwa kama lengo kuu la Mkakati wa Afya wa Afrika toka 2016- 2030 (AHS) ambapo dawa Muhimu, Usalama wa Bidhaa na Mifumo ya Ugavi inafafanuliwa kama utaratibu wa kimkakati ya AHS. Miongoni mwa idadi ya watu wenye afya na tija ya bara hili, ni upatikanaji wa dawa salama, bora na za bei nafuu, bidhaa za matibabu na teknolojia – kama nguzo kuu ya Huduma ya Afya kwa Wote.

3. Barani Afrika, upatikanaji wa dawa salama, na bora, bidhaa za matibabu na teknolojia bado ni mdogo. Hii kwa kiasi kikubwa ni kutokana na udhaifu na ufanisi duni pamoja na mifumo na michakato ya udhibiti iliyoparaganyika. Mifumo na michakato ya udhibiti iliyoparaganyika imechangia kuchelewesha watafiti na watengenezaji wa bidhaa za dawa, ambao lazima wapitie mifumo mingi ya udhibiti ili kusajili bidhaa ileile ya afya katika nchi nyingi wanachama.

4. Kwa upande mwingine, mifumo dhaifu na isiyo na tija ya udhibiti imesababisha kuenea kwa usambazaji wa dawa zisizo na viwango na feki (SF) pamoja na dawa hatari, bidhaa za matibabu na teknolojia ya afya katika nchi nyingi wanachama wa AU. Uuzaji na utumiaji wa dawa za SF umeleta tishio kubwa kwenye kuhakikisha afya ya umma ya bara la Afrika. Ubaya wake umejionesha kijamii na kiuchumi. Kwa mfano, vifo kadhaa viliripotiwa kutokana na utumiaji wa dawa za SF, matokeo ya kiafya kama vile kuficha dalili za magonjwa na ukinzani wa dawa, na kupoteza imani ya umma katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya. Zaidi ya hayo, pia imeongeza matumizi ya huduma za afya nje ya bajeti kwa magonjwa yanayotokana na utumiaji wa dawa za SF, imepoteza mapato ya serikali kutokana na ushuru ambao haujalipwa na matumizi makubwa ya serikali kukabiliana na tishio hilo.

5. Kutokana na hali hii, Halmashauri Kuu ya AU mnamo Januari 2015, ilitambua hitaji la kuimarisha uwezo wa udhibiti wa bidhaa za matibabu na kuoanisha mifumo ya udhibiti barani Afrika, kama msingi wa kuanzishwa kwa wakala mmoja wa udhibiti wa dawa barani Afrika, katika muktadha huo wa Mpango wa Kuoanisha Dawa za Kiafrika (AMRH), na sehemu ya Mpango wa Utengenezaji wa Dawa kwa Afrika (PMPA) (EX.CL/Dec.857 (XXVI)). Ikumbukwe, Mkakati wa Afya wa Afrika wa mwaka 2016-2030 pia unaangazia hili kama mojawapo ya taratibu zake za kimkakati, ujenzi wa mazingira imara ya udhibiti ili kusaidia utoaji wa dawa na teknolojia salama na bora ikiwa ni pamoja na kukuza Tiba ya Asili ya Kiafrika.

6. Kwa muktadha huo, Baraza Kuu liliidhinisha hatua muhimu za AMA na kuitaka Kamisheni, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika-NEPAD na Shirika la Afya Duniani kwa kushirikiana na wadau wengine kufafanua wigo wa dawa, bidhaa za matibabu na teknolojia zitakazoshughulikiwa na majukumu ya AMA, na kutayarisha mbinu za kina, mfumo wa kitaasisi, athari za kisheria na kifedha, za kuanzishwa kwa AMA. Ni katika muktadha huu ndipo Mkataba wa AMA ulipopitishwa na Wakuu wa Nchi za Afrika mnamo Februari 2019 (Assembly/AU/Des.735 (XXXII)) na kuanza kutumika tarehe 5 Novemba 2022 kufuatia kuwekwa kwa hati ya 15 ya uidhinishaji`

## III. Hatua ya Utiaji saini na Kuidhinishwa kwa Mkataba wa AMA

7. Kufikia tarehe 24 Novemba 2023, nchi wanachama thelathini na tatu (33) zimetia saini Mkataba wa AMA huku nchi wanachama ishirini na sita (26) zimeridhia na kuweka hati ya kisheria ya kuridhia kwenye Tume. Jedwali la 1 linaonyesha idadi na nchi wanachama ambazo zimetia saini na kuridhia Mkataba wa AMA kufikia tarehe 31 Desemba 2022.

**Jedwali la 1: Hatua ya Kutiwa saini na Kuidhinishwa kwa Mkataba wa AMA kufikia tarehe 24 Novemba 2023**

| Nchi Wanachama ambazo zimetia saini : 33 | Nchi Wanachama ambazo zimeridhia: 26 |
|---|---|
| 1. Algeria | 1. Algeria |
| 2. Benin | 2. Benin |
| 3. Burundi, | 3. Burkina Faso* |
| 4. Cabo-Verde | 4. Cabo-Verde |
| 5. Cameroon | 5. Cameroon |
| 6. Chad | 6. Chad |
| 7. Comoros | 7. Congo |
| 8. Egypt | 8. Egypt |
| 9. Republic of Congo | 9. Gabon |
| 10. Cote d'Ivoire | 10. Ghana |
| 11. Equatorial Guinea | 11. Guinea |
| 12. Ethiopia | 12. Kenya |
| 13. Gabon | 13. Lesotho* |
| 14. Ghana | 14. Mali |
| 15. Guinea | 15. Mauritius |
| 16. Kenya | 16. Morocco |
| 17. Mali | 17. Namibia* |
| 18. Mauritius | 18. Niger |
| 19. Morocco | 19. Rwanda |
| 20. Madagascar | 20. Saharawi |
| 21. Mozambique | 21. Senegal |
| 22. Niger | 22. Seychelles |
| 23. Rwanda | 23. Sierra Leone |
| 24. Saharawi | 24. Tunisia |
| 25. Sao Tome and Principe | 25. Uganda |
| 26. Senegal | 26. Zimbabwe |
| 27. Seychelles | |
| 28. Sierra Leone | (* Kuridhia bila kutia saini) |
| 29. Tanzania | |
| 30. Tunisia | |
| 31. Togo | |
| 32. Uganda | |
| 33. Zimbabwe | |

## IV. Uendeshaji wa AMA

8. Tume ya AU imepiga hatua katika kuharakisha utendakazi wa AMA. Hatua kuu zilizofikiwa ni pamoja na;

- Uwasilishaji wa Ripoti ya Maendeleo ya AMA ya 2022 kwenye Bunge la Umoja wa Afrika mnamo Februari 2023 na kupitishwa kwa Taratibu za Uteuzi za Bodi ya Utawala ya AMA;
- Kutiwa saini kwa Mkataba wa Nchi Mwenyeji wa Makao Makuu ya AMA tarehe 10 Juni 2023;

- Kikao cha Pili Maalum cha Mkutano wa Nchi Wanachama juu ya Mkataba wa AMA: 19-20 Juni 2023;
- Kuanzishwa kwa Bodi ya Utawala ya AMA;
- Warsha ya Uhamasishaji wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda kuhusu Uendeshaji wa AMA, tarehe 10 Julai 2023;
- Kampeni za Uchechemuzi kwa ajili ya Kuongeza nchi zinazoridhia mkataba wa AMA.

**a) Uwasilishaji wa Ripoti ya Maendeleo ya AMA mnamo 2022 kwenye Bunge la Umoja wa Afrika mnamo Februari 2023**

9. Mkutano wa 37 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mnamo Februari 2023 ulipitisha Ripoti ya Maendeleo ya uanzishaji na uendeshaji wa AMA pamoja na Taratibu za Uteuzi wa Bodi ya Utawala ya AMA na hatua muhimu juu ya nini kifanyike.

**b) Utiaji saini wa Mkataba wa Nchi Mwenyeji wa Makao Makuu ya AMA tarehe 10 Juni 2023**

10. Kuendelea kwa Uamuzi wa Kikao cha 41 cha Kawaida cha Baraza Kuu EX.CL/Dec.1179(XLI) kwa mujibu wa uamuzi wa Halmashauri Kuu /AU/Des. 830(XXXV), kuidhinisha Baraza Kuu kuchukua uamuzi kwa niaba ya Halmashauri Kuu kwaajili ya Mwenyeji wa Makao Makuu ya AMA, Makao Makuu ya AMA yaliamuliwa kuwa nchini Rwanda. Kwa hiyo, Tume, kupitia ofisi yake ya wataalamu wa sheria imeshirikiana na Serikali ya Rwanda kukamilisha rasimu ya Mkataba wa Mwenyeji wa Makao Makuu ya AMA. Mara baada ya kukamilika, Tume na Serikali ya Rwanda zilitia saini rasimu ya Mkataba wa Mwenyeji wa Makao Makuu ya AMA tarehe 10 Juni 2023, mkataba wa mwenyeji ambao baadaye uliidhinishwa na Bunge la Rwanda mnamo Oktoba 2023.

**c) Kikao cha Pili Maalum cha Mkutano wa Nchi Wanachama wa AMA: tarehe 19-20 Juni 2023**

11. Kwa mujibu wa mapendekezo ya Kikao cha Kwanza Maalum cha Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa AMA uliofanyika kuanzia tarehe 3-4 Novemba 2022 uliamua kwamba kikao cha pili Maalum kijadili: a) Uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Uongozi ya AMA. na Kujadili na kupitishwa kwa Hadidu za Rejea za Mkurugenzi Mkuu, Tume iliandaa Kikao cha Pili Maalum cha Mkutano wa Nchi Wanachama wa AMA (CoSP) kuanzia tarehe 19 - 20 Juni 2023. Katika Kikao hiki, CoSP ilipewa taarifa kuhusu hatua ya Maendeleo ya uanzishaji na uendeshaji wa AMA ikijumuisha lakini sio tu uanzishwaji wa Bodi ya Uongozi ya AMA. Zaidi ya hayo, CoSP ilipitisha Majukumu na kazi za Mkurugenzi Mkuu wa AMA.

12. Hata hivyo, uanzishwaji wa Bodi ya Uongozi ya AMA uliahirishwa na CoSP kwa sababu kati ya mapendekezo 7 yaliyopokelewa ya wajumbe wa Bodi ya Uongozi ya AMA, matatu (3) kati yao yanakidhi kigezo na manne (4) kati yao hayakidhi kigezo cha Bodi ya AMA. Katika suala hili, uingizwaji wa wasifu wa kutosha na uzoefu unaofaa unahitajika ili kuimarisha uwezo wa AMA kufanya kazi kwa umahiri na kufikia malengo yake. Zaidi ya hayo, Jumuiya za Uchumi za Kikanda za Kati na Kaskazini zilihimizwa kukamilisha mashauriano na kutuma wateule wao hivi karibuni ifikapo tarehe 3 Agosti 2023.

13. Kutokana na hali hii, CoSP ilipendekeza kuanzishwa kwa kamati ya dharura itakayoshirikiana na Tume ya AU kushauriana na jumuiya za Kikanda ili kutathmini wasifu uliowasilishwa. Kwa hiyo, CoSP iliziomba nchi Wanachama wa ofisi ya AMA (tazama jedwali hapa chini) kusimamia mchakato huu kwa msaada wa AUC, NEPAD na Africa CDC.

**Jedwali la 2: Uwakilishi wa Ofisi ya AMA**

| **Kanda** | **Nchi Mwanachama** | **Nafasi/ Cheo** |
|---|---|---|
| Afrika Magharibi | Jamhuri ya Ghana | Mwenyekiti |
| Afika ya Kati | Jamhuri ya Tchad | Makamu Mwenyekiti |
| Afrika ya Kati | Jamhuri ya Uganda | Makamu Mwenyekiti wa |
| Afrika ya Kaskazini | Anatarajia Kuthibitish baadaye | Makamu Mwenyekiti Tatu |
| Kusini mwa Afrika | Jamhuri ya Namibia | Mjumbe maalum |

14. Wakati wa Kikao cha Pili Maalum cha AMA, CoSP ilipendekeza yafuatayo kama vipengele vya ajenda kwenye kikao chake cha tatu maalum:

i) Kupitishwa kwa Bodi ya Uongozi ya AMA;

ii) Taratibu za Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa AMA na;

iii) Kupitisha Muundo muhimu wa AMA.

d) Kuanzishwa kwa Bodi ya Uongozi ya AMA

| Jina | Wasifu | Nchi/Taasisi | Mawasiliano |
|---|---|---|---|
| 1. 1. Kanali Dkt Yossounon Chabi, | Mkurugenzi Mkuu, Wakala wa Udhibiti wa Dawa wa Benin | Benin kwa Kanda ya Magharibi | chabivoss@yahoo.fr |
| 2. Germina Mamoeti Mphoso | Mkuu wa Mamlaka ya Famasia na Udhibiti wa Wizara ya Afya (MOH) | Lesotho kwa Kanda ya Kusini mwa Afrika | y nn, gmphoso@yahoo.com |
| 3. Dkt. Emile Bienvenu | Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Rwanda (RFDA) | Rwanda kwa nchi za Afrika Mashariki | dg@rwandafda.gov.rw |
| 4. Dkt. Haoua Haroun Saker | Naibu Mkurugenzi wa Famasia na Dawa | Tchad, kwa Kanda ya Afrika ya Kati | haouasaker@yahoo.fr |
| 5. MHE. Balozi Minata Samate Cessouma | Kamishna wa Afya, Masuala ya Kibinadamu na Maendeleo ya Jamii | AUC | |
| Inasubiri | | | |
| Itafahamika | Kanda ya Afrika ya Kaskazini | Barua ya kukumbushia ilitumwa | |
| Itafahamika | CEN-SAD | Barua inaandaliwa<br><br>CEN-SAD iliripoti kwenye Tume kupitia barua rasmi kwamba haina uwezo ulioombwa, lakini ilikabidhi Mamlaka ya Madawa ya Misri kuwawakilisha. Kisha baada ya hapo, Moroko ilituma Ujumbe kwenye Tume ikidai kuwa wanawakilisha CEN-SAD. Tume iliomba CENSAD kufanya mashauriano na kuwasilisha jina la mtu anayewakilisha | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | CENSAD haraka iwezekanavyo. | |
| Itafahamika | ECCAS | ECCAS na WAHO wako katika harakati za kumteua mwakilishi wao. | |
| Itafahamika | Shirika la Afya la Afrika Magharibi (WAHO) | | |

15. Kwa mujibu wa hitimisho na mapendekezo ya Mkataba wa 2 wa CoSP kwenye Mkataba wa AMA, Tume iliamua kufanya mawasiliano zaidi (kupitia Note Verbales na Barua) kwa Nchi Wanachama, Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda ambazo zilipaswa kujibiwa ndani ya mwezi mmoja. Tarehe ya mwisho imeisha, na Tume imetuma barua lakini hadi sasa, kuna teuzi mbili tu za ziada ambazo zinafanya idadi ya sasa ya wanachama kuwa 5 ikiwa ni pamoja na Tume yenyewe.

Tazama jedwali hapa chini

e) Warsha ya Uhamasishaji wa Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda (RECs na RHOs) juu ya Uendeshaji wa AMA, 10 Julai 2023

16. Zaidi ya changamoto zilizojitokeza na Uteuzi wa Bodi ya Uongozi ya AMA na majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa na RECS na RHOS, Tume iliandaa warsha ya uhamasishaji mtandaoni na Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda zote zinazotambuliwa na AU mnamo tarehe 10 Julai 2023. Warsha hiyo iliipa fursa AUC kutoa muhtasari wa Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda kuhusu hali ya maendeleo ya ufanisi wa AMA lakini pia kujadili jinsi Jumuiya hizo za Kiuchumi za Kikanda na Vyombo hivyo vya Afya vya Kikanda zinaweza kuharakisha michakato ya Bodi ya Utawala ya AMA.

f) Uchechemuzi wa AMA kuhusu Ongezeko la nchi zinazoridhia Mkataba

17. Zaidi ya Uamuzi wa Kikao cha 41 cha Kawaida cha Baraza Kuu EX.CL/Dec.1179(XLI) "UNAHIMIZA Nchi Wanachama ambazo zimetia saini Mkataba wa AMA kuuridhia na UNATOA WITO kwa Nchi nyingine Wanachama kutia saini na kuridhia Mkataba huo. kulinda afya ya umma, usalama na kuimarisha upatikanaji wa dawa bora, salama na zenye ufanisi na bidhaa za matibabu katika bara hili" Tume imependekeza Hadidu za Rejea na mpango wa uchechemuzi wa ngazi ya juu kwa Mhe. Michel Sidibe Mjumbe Maalum wa AMA. Lengo ni kufufua juhudi za uchechemuzi kuhusu ongezeko la utiaji saini na uridhiaji wa mkataba wa AMA. Mpango huo unafanyiwa mapitio ili ujumbe wa ngazi ya juu uanze katika robo ya kwanza ya 2024 kwa ziara ya kwanza katika nchi 7 pamoja na Jumuiya za Uchumi za Kikanda kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na warsha ya uhamasishaji ya Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda.

## V. Ombi la Kuwa Mwenyeji wa Vituo vya Kanda vya Ubora wa Udhibiti wa AMA (RCOREs)

18. Nchi mbili Wanachama zimeonyesha nia ya kuwa mwenyeji wa RCORE. Ombi la kwanza liliwasilishwa na Jamhuri ya Zimbabwe wakati wa Kikao cha Kwanza cha Kawaida cha Mkutano wa Nchi Wanachama mwezi Juni 2022. Tume ilipokea ombi la pili la kuwa Mwenyeji kutoka Jamhuri ya Mauritius.

19. Tume inapokea maombi hayo ya kuwa mwenyeji. Kwa vile Tume sasa iko katika mchakato wa kushughulikia utendakazi wa AMA, wagombea wa RCORE bado hawajazinduliwa rasmi. Katika muda ufaao maombi hayo ya kuwa mwenyeji yatawasilishwa kwenye Mkutano wa Nchi Wanachama ili kuamua, kwa mujibu wa mkataba wa AMA na kanuni zake za utaratibu.

‘

**Msaada kwa ajili ya Uendeshaji wa AMA**

### a. AUDA-NEPAD na Africa CDC

20. Afrika CDC na AUDA-NEPAD zilitoa msaada wa kiufundi na kifedha kwenye tume kama sehemu ya juhudi za uratibu wakati wa mchakato wa uendeshaji wa AMA.

### b. Msaada kutoka Shirika la Afya Duniani

21. Kwa mujibu wa Mkataba wa Makubaliano wa AUC/WHO wa tarehe 18 Novemba 2019, Shirika la Afya la Duniani lilikubali kuendelea kuunga mkono ajenda ya Uchechemuzi ya Tume kwa kiasi cha USD 200,000 ili kuongeza idadi ya nchi zinazoridhia Mkataba wa Wakala wa Dawa wa Afrika (AMA).

### c. Wakfu wa Bill na Melinda Gates

22. Wakfu wa Bill na Melinda Gates - ulionyesha nia ya kuunga mkono shughuli za AMA na umetoa msaada wa kifedha kwa mwaka 2023. Taratibu za usaidizi na maeneo ya ushirikiano zimekubaliwa na kuainishwa katika Rasimu ya Makubaliano na Makubaliano kutiwa saini. Sehemu ya msaada wa kifedha ilitumika kulipia gharama ya kuandaa Mikutano mikuu miwili:

i) Mkutano wa Pili Maalum wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa AMA na;

ii) na Mkutano wa Uchechemuzi wakati wa Mkutano wa 73 wa UNGA uliopewa jina la ‘’ Advancing Pandemic Prevention, Preparedness and Response (PPPR) yaani Kuweka Mifumo ya Kuzuia Magonjwa ya Kuambukizwa, Maandalizi na Mwitikio (PPPR) na Utengenezaji wa ndani wa madawa na teknolojia za afya barani Afrika, Kutumia mchango wa Mashirikiano/ubia kati ya sekta za umma na binafsi’’.

### d. **Changamoto**

23. Tume imepata changamoto tatu kuu katika kuendeleza utendakazi wa AMA:

i. Changamoto ya kwanza inahusu mwitikio wa polepole sana na uliocheleweshwa kutoka Nchi Wanachama wa AU, RECs na RHOs kuhusu uanzishwaji wa Bodi ya Utawala ya AMA. Hii imesababisha kuchelewa kuikamilisha bodi;

ii. Changamoto ya Pili inahusiana na bajeti ya shughuli za AMA. Tume imetegemea kwa ujumla misaada ya washirika wa nje ili kufanya shughuli zinazohusiana na AMA mwaka 2023. Kwa hivyo Tume imekumbana kidogo na mara nyingi ililazimika kutegemea misaada ya washirika.

iii. Changamoto ya tatu inahusiana na ukosefu wa uwezo. Kurugenzi ya Masuala ya Afya na Kibinadamu haina wafanyakazi kamili walioajiriwa kwa ajili ya uendeshaji wa AMA, hali ambayo ilichangia kucheleweshwa kwa utekelezaji wa shughuli za AMA.

e. **Hatua zinazofuata na nini kifanyike**

i) Kuendelea na harakati za uchechemuzi juu ya haja ya Utiaji saini na kuridhia Mkataba wa AMA baina ya nchi wanachama wa AU;

ii) Kukamilika kwa michakato ya uteuzi wa Bodi ya Utawala ya AMA na CENSAD, ECCAS na WAHO. Kuhusu CENSAD, Tume pia imeomba ushauri wa kisheria na imeshauriwa ipasavyo. Hatua inayofuata itakuwa kwa CEN-SAD kutuma jina la mteule kwenye Tume;

iii) iii. Kukamilika kwa Muundo wa AMA na taratibu za Michango ya Kifedha;

iv) iv. Kuandaa Kikao cha 3 Maalum cha Mkutano wa Nchi Wanachama;

v) v. Kuandaa Kikao cha Kwanza cha Kawaida cha Bodi ya Uongozi ya AMA katika robo ya kwanza ya 2024 ili kupitisha sheria zao na kujadili zaidi michakato muhimu kuhusu Muundo wa AMA na Taratibu za Ajira ya Mkurugenzi Mkuu;

vi) vi. Kuendelea kushirikiana na Serikali ya Rwanda ambayo ni Mwenyeji wa AMA ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Mkataba;

vii) vii. Kuteuliwa kwa timu maalum kutoka idara muhimu za AUC zinazohusika na uendeshaji na kuhamishiwa kwa muda kwenye Makao Makuu ya AMA kwa lengo la kusaidia mchakato wa kuanzishwa kwa ofisi husika.

**SEHEMU YA 2. RASIMU YA UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO YA WAKALA WA DAWA AFRIKA (AMA) 2023.**

**Halmashauri Kuu,**

1. **INAPOKEA** ya Ripoti ya Maendeleo ya Wakala wa Dawa wa Afrika (AMA) ya 2023 na mapendekezo yaliyomo.

2. **PIA INAPOKEA** changamoto ambazo Tume imekumbana nazo zinazohusiana na mrejesho kutoka kwa Nchi Wanachama, Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo ya Afya vya Kikanda wakati wa kuanzisha Bodi ya Uongozi ya AMA;

3. **INATOA WITO** kwa jumuiya za Uchumi za Kikanda na Vyombo vya Afya vya Kikanda ambazo bado hazijateua mgombea, hazijakamilisha mashauriano na kutuma kwenye Tume ili kujadiliwa kwenye Bodi ya Uongozi ya AMA.

4. **INAKARIBISHA** kutiwa saini na kuridhiwa kwa Makao Makuu ya Mkataba wa AMA kati ya Tume na Serikali ya Rwanda pamoja na kupitishwa kwa Kazi na Majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa AMA na Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa AMA.

5. **INAIPONGEZA** Tume, AUDA-NEPAD, Africa CDC, Ofisi ya AMA na Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa AMA kwa maendeleo yaliyofikiwa licha ya kukumbana na changamoto nyingi katika uanzishaji na uendeshaji wa AMA;

6. **PIA INAZIPONGEZA** nchi 26 ambazo zimeridhia Mkataba wa AMA na kuzitaka nchi zilizosalia kwa zile zilizotia saini mkataba huo kuridhia na zilizosalia kutia saini na kuridhia.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository http://archives.au.int

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-02-15

# Progress Report on the establishment and operationalization of the African Medicines Agency

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10524

*Downloaded from African Union Common Repository*